
# Ushirikiano wa elimu mjumuisho kwa Mashirika ya Watu Wenye Ulemavu

Moduli ya

**2**



## Kitabu cha Washiriki


Umetayarishwa kwa ajili ya:

Jumuiya ya MECP-Z na Jumuiya za Watu wenye Ulemavu

The Norwegian Association of Disabled

Umeandaliwa na:

Enabling Education Network

NAD – The Norwegian Association of Disabled

MADRASA EARLY CHILDHOOD PROGRAMME

EENET

Inclusive Learning Approach

[Ufafanuzi wa picha (picha ya jalada)]: Watu watano wamekusanyika nje chini ya mti, wanne wamekaa juu ya vibao na mmoja amesimama. Watatu ni wanawake na wawili ni wanaume. Wanawake wawili wamevaa hijabu na mwanamme mmoja amevaa kanzu. Wote wanamsikiliza mwanamme aliyesimama ambae anazungumza. Mtu huyo amevaa suti, ana mguu mmoja na anatumia gongo la kutembelea. Kando yake kuna flipchati iliyowekwa kwenye stendi ikiwa na michoro ya watu wawili – mtoto wa kiume na mtoto wa kike wakiwa ndani ya nyumba ilioezekwa bati. Upande mwengine wa flipchati kuna mwanamke aliyesimama akitoa ishara za lugha ya alama. Wote wawili, mwanamke na mwanamme wamewaelekea watu watano wanaowasikiliza].

Unaruhusiwa kusambaza na kusanifu muongozo huu ili uendane na mazingira uliopo. Hata hivyo unapaswa kutoa utambulisho sahihi, chimbuko la idhini, na uoneshe iwapo kuna mabadiliko uliyoyafanya. Unaweza kufanya hivyo kwa namna yoyote inayokubalika, lakini bila kuonesha kuwa mabadiliko au matumizi hayo yamethibitishwa na taasisi inayohodhi haki ya muongozo huu. Huruhusiwi kutumia muongozo huu kwa lengo la kujinufaisha kibiashara. Iwapo utauhariri muongozo huu, kuurekebisha, au kuongezea kilichoandikwa humu, utapousambaza unapaswa kutumia idhini halisi kama iliotumika kabla ya muongozo kufanyiwa marekebisho. Huruhusiwi kutumia kanuni za kisheria au teknolojia ambayo kisheria itawazuia wengine kufanya chochote katika muongozo huu ambacho idhini ya awali imeruhusu. Kwa taarifa zaidi, rejea kwenye kiungo kifuatacho:
https://creativecommons.org/licenses/by-nc-sa/4.0/legalcode

Miongozo hii inapatikana chini ya Leseni ya Creative Commons Non-Commercial 4.0 International

# Contents

Vifupisho .... 4
Kitabu hiki ni cha nini na kwa ajili ya nani? .... 5
1. Nini maana ya Kamati ya Elimu mjumuisho ya Skuli (SIT)? .... 6
2. Mkabala wa mbinu pacha .... 11
3. Simulizi ya Yussuf .... 12
4. Tunawezaje kushirikiana kuisaidia skuli kuwa jumuishi zaidi? .... 20
5. Kufahamu mahusiano ya kimadaraka .... 21
6. Ushirikiano na kamati ya elimu mjumuisho ya skuli .... 27
7. Jukumu la mratibu wa elimu mujumuisho wa skuli (IECo) .... 28
8. Fursa za ushirikiano katika jamii zetu .... 32
9. Kutoka matatizo hadi rasilimali .... 36
10. Jinsi ya kutengeneza ramani ya rasilimali za jamii .... 41

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| IEP | Mpango binafsi wa kielimu |
| EENET | Enabling Education Network |
| NAD | Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu ya Norway |
| NGO | Jumuiya isiyo ya kiserikali |
| SIT | Kamati ya elimu mjumuisho ya skuli |
| ToT | Mafunzo kwa ajili ya Wakufunzi |

# Kitabu hiki ni cha nini na kwa ajili ya nani?

Kitabu hiki ni kwa ajili ya washiriki kutoka katika jumuiya za watu wenye ulemavu (JWU) kikiwa ni moduli ya 2 katika mafunzo yanayohusu elimu mjumuisho.

Lengo la moduli hii ni kuzisaidia jumuiya za watu wenye ulemavu (JWU) na wanachama wao kutafakari ni nani wanahitaji kushirikiana nae ili kujenga skuli ambazo ni jumuishi katika jamii zao. Hii ikiwemo kuzingatia ni nani JWU zinahitaji kumkabili, na kuzisaidia skuli kuunda na kuzisimamia kamati za elimu mjumuisho za skuli (SIT). Kitabu hiki pia kimezingatia jinsi ya kutambua rasilimali muhimu na uwezo uliopo katika jamii zao na kuzitumia rasilimali hizo kujenga mtandao imara utakaosaidia elimu mjumuisho.

Mafunzo haya ni sehemu ya mchakato wa muda mrefu wa kuzijengea uwezo JWU, na mafunzo ya ziada yataandaliwa kuendeleza kile kilichofundishwa katika mafunzo haya.

Elimu mjumuisho **sio** tu kuwaandikisha watoto wenye ulemavu skuli. Bali ni kuhakikisha kwamba kila mwanafunzi **anahudhuria** skuli, **anashiriki** katika kujifunza na harakati za kijamii, na **anafaulu** hadi kufikia ukomo wa uwezo wake wa kujifunza

# 1. Nini maana ya Kamati ya Elimu mjumuisho ya Skuli (SIT)?

Kamati ya elimu mjumuisho ya skuli (SIT) inahusisha kikundi cha watu wanaojitolea ambao wana lengo la kuimarisha sekta ya elimu au kuimarisha skuli yao na wenye lengo linalowaunganisha pamoja– kuifanya skuli yao iwe jumuishi zaidi.




*Mfano wa mkutano wa kamati ya elimu mjumuisho ya skuli iliyokutana katika viwanja vya skuli*

[Ufafanuzi wa picha: Kuna watu nane waliokaa nje chini ya mti katika umbo la nusu duara. Wamekaa kwenye viti. Nyuma yao kuna skuli na watoto wanacheza nje ya skuli hiyo. Kuna wanawake watatu katika kikundi cha watu waliokaa, mmoja amevaa hijabu. Kuna mtu mwengine amekaa kwenye kitimwendo na mzee aliyeshika fimbo ya kutembelea. Kuna mtu mwengine katika kikundi ambae anatoa ishara za lugha ya alama. Mwanamke mwengine anazungumza huku akiashiria. Kando yake kuna gongo la kutembelea.]

## Visa mafunzo – nini maana ya kamati za elimu mjumuisho za skuli?

**Soma visa mafunzo vifuatavyo. Unadhani kila kisa kinaelezea maana ya kamati ya elimu mjumuisho ya skuli? Kwa nini?**

**Kisa mafunzo A**

Kila baada ya miezi 3, walimu 3 wa madarasa katika skuli ndogo iliyopo kijijini hukutana kujadili changamoto zinazowakabili katika kuwafundisha wanafunzi wenye ulemavu walioandikishwa katika skuli hiyo. Walimu wengine wawili katika skuli hiyo hawapo tayari kujumuika na walimu hawa katika vikao, na hakuna mtu yeyote aliyewashawishi kushiriki katika vikao hivyo.

**Kisa mafunzo B**

Katika skuli kubwa, kuna timu iliyoundwa ili kuandaa mipango binafsi ya kielimu (IEP) kwa wanafunzi 30 ambao walibainika kuwa na mahitaji maalumu katika kujifunza. Timu hiyo inajumuisha mtaalamu wa mbinu za kufundishia, mwanasaikolojia, walimu wawili wa madarasa, na wataalamu 3 wa elimu mjumuishi kutoka nje ya skuli.

**Kisa mafunzo C**

Kila mwaka, Skuli C huitisha mkutano mmoja unaojumuisha wazazi wote/walezi. Katika mkutano huu, mwalimu mkuu huwaeleza wazazi/walezi kuhusu sera ya skuli ya elimu mjumuisho, akiwaomba kuhakikisha kwamba watoto wote wanahudhuria skuli, na kuwaambia kile ambacho walimu na wataalamu maalum wamekuwa wakikifanya ili kuwasaidia wanafunzi waliobainika kuwa na mahitaji maalum katika kujifunza.

**Kisa mafunzo D**

Skuli D ina wanafunzi tofauti, wakiwemo wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika kujifunza/ulemavu na wanafunzi kutoka katika makabila matatu tofauti. Baadhi ya walimu, wazazi/walezi na wataalamu hukutana kila baada ya wiki mbili kujadili changamoto mpya zilizoibuka katika ujumuishaji, na kutathmini maendeleo na kutatua changamoto. Hivi sasa wapo katika mchakato wa kuwajumuisha wawakilishi wawili wa wanafunzi katika kikundi hicho, ili wapate mawazo kutoka kwa wanafunzi wenyewe na kusaidia katika kuwatambua wanafunzi wengine ambao hawahudhurii skuli.

**Kisa mafunzo A: Je, hii ni kamati ya elimu mjumuisho ya skuli?**

- Ndio… kwa sababu hakuna muongozo maalumu kuhusu wajumbe wa kamati au wakutane mara ngapi, kwa hivyo si lazima kuwa na idadi maalum, kwa mfano, kamati haina mtaalamu maalumu (inawezekana skuli haina mtaalamu wa mbinu za ufundishaji au mwanasaikolojia) au wataalamu kutoka nje, au kwamba wanakutana mara nne tu kwa mwaka.
- Hapana… kwa sababu timu inaonekana kushughulika na masuala ya ulemavu tu – na hususani kwa aina maalumu ya wanafunzi kuliko masuala mengine ya kimfumo – bila ya kuzingatia changamoto nyengine za ujumuishwaji (mf., vijijini kunaweza kuwa na changamoto za ufukara, usafiri wa kwenda skuli, n.k.)
- Hapana… kwa sababu hakuna juhudi zilizochukuliwa kuwasiliana na walimu wengine na pia labda hakuna jitihada zozote zilizochukuliwa kukuza uwelewa wao kuhusu elimu mjumuisho.

**Kisa mafunzo B: Je, hii ni kamati ya elimu mjumuisho ya skuli?**

- Hapana… kwa sababu dhamira ya timu imejikita katika eneo dogo. Inaadaa mipango kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu tu. Haionekani kufanya kazi katika uwanda mpana wa masuala ya ujumuishaji kwa wanafunzi hawa au wanafunzi wengine wanaokabiliwa na vikwazo katika elimu.
- Hapana… kwa sababu wajumbe wake wengi ni wataalamu tu, sio walimu wa kawaida, walimu wa elimu mjumuisho na wadau wengine.

- **Kisa mafunzo C: Je, hii ni kamati ya elimu mjumuisho ya skuli?**
- Hapana… kwa sababu ingawa kuna uhusishwaji wa wazazi/walezi, lakini sio shirikishi. Wazazi/walezi wanaambiwa tu kinachoendelea, lakini hawaalikwi kushiriki kikamilifu katika harakati za skuli za ujumuishaji (kubaini changamoto na kuzitatua).

- **Kisa mafunzo D: Je, hii ni kamati ya elimu mjumuisho ya skuli?**

- Ndio… kwa sababu inahusisha wadau mbalimbali, na inashughulikia changamoto mbalimbali za ujumuishaji.

# Muhutasari wa maana ya kamati ya elimu mjumuisho ya skuli


## Kamati ya elimu mjumuisho ya skuli:

- huwaleta pamoja wadau wa elimu au walio karibu na skuli na wenye **lengo linalowaunganisha** – kuifanya skuli yao iwe jumuishi zaidi;
- ina wawakilishi tofauti **wanaofanya kazi kwa kujitolea;**
- inaweza **kujumuisha wataalamu wasiohusika na elimu** na vile vile wafanyakazi wa skuli, walimu, mafundi wa ujenzi, wafanyakazi wa sekta ya afya, wanachama wa JWU n.k.
- **ipo kwa ajili ya kuwasaidia** walimu, wafanyakazi wengine, wanafunzi na wazazi/walezi – sio kuongeza ngazi nyengine ya urasimu au mzigo. Iwapo kamati itageuka mzigo au kufanya kazi kama chombo chenye urasimu, itakuwa inakwenda kinyume na malengo yaliyokusudiwa;
- inapaswa kuwa mfano wa maana halisi ya ujumuishi, **na kutoa msaada kiutekelezaji na ushauri** ili wengine waigeuze elimu ya nadharia ya ujumuishi kuwa uhalisia;
- Hushughulika na **changamoto zote za ujumuishaji wa skuli** ambazo zinaweza kujitokeza katika nyakati tofauti katika kipindi cha mwaka wa masomo – kwa mfano, sababu na suluhisho kwa matokeo ya unyanyasaji dhidi ya wanafunzi wengine, utoro au uchelewaji – mambo ambayo ni kikwazo kwa ujumuishi.




Ramani ya kumbukumbu iliyotayarishwa na washiriki wa Zanzibar

[Ufafanuzi wa picha: Ramani ya mawazo, duara lililopo katikati lina neno Kamati ya elimu Mjumuisho. Kuna mishale mitatu yenye maelezo kuhusu ‘kazi za Kamati ya Elimu Mjumuisho’; mitatu ikielezea ‘changamoto’; na miwili ikielezea ‘suluhisho’. Kila mshale umeunganishwa katika duara kubwa].




Mchoro wa Kamati ya elimu mjumuisho uliobuniwa na washiriki wa Zanzibar

[Ufafanuzi wa picha: Picha inaonesha mchoro wa baiskeli chini ya kichwa cha habari 'Baiskeli ya kamati ya elimu mjumuisho ya skuli!'. Sehemu mbalimbali za baskeli ni pamoja na maringi, kibao cha kukalia, sukani n.k. ambazo zimepewa majina ya 'wanafunzi', 'viongozi wa kiraia', 'jamii (wazazi), Wizara ya Elimu/Afya, 'jumuiya ya wafanya biashara']

## 2. Mkabala wa mbinu pacha

Elimu mjumuisho inalenga kubadilisha mfumo na sio kumbadilisha mwanafunzi. Hata hivyo, kwa kuzingatia mabadiliko ya kiwango cha mfumo, haimaanishi kwamba tunapaswa kupuuza mahitaji **mahususi** ya **kila** mwanafunzi.

Tunahitaji kukabiliana na mitazamo ya kutotiliwa maanani kwa Elimu Mjumuisho katika **namna mbili**: Namna hizo ni kuimarisha mabadiliko ya kimfumo **na** kwa kutoa msaada maalumu kulingana na mahitaji ya kujifunza kwa kila mwanafunzi.
Hii ndio inaitwa **mbinu pacha**.

**Cha kuzingatia kwenye mfumo**
Kuhakikisha, mazingira ya kufundishia na kujifunzia, mitazamo pamoja na mbinu zinalenga kukabiliana na tafauti na kuimarisha ujumuishaji pamoja na kuondoa vikwazo.

**Cha kuzingatia kwa mwanafunzi:**
Kuheshimu maoni yao na kuwapatia msaada unaofaa kama ilivyo haki yao. Hii itapelekea kuwawezesha kupitia kuwepo, kushiriki na mafanikio yao.

**Elimu mjumuisho**
Kukabiliana na tafauti

Soma **simulizi ya Yussuf** na angalia iwapo unaweza kupata mifano ya:

- Hatua zinazolenga **kubadilisha mfumo,** au kufanya mabadiliko katika skuli nzima au darasa zima
- Hatua zinazolenga **kutoa usaidizi wa mwanafunzi mmoja mmoja** kwa mtoto mmoja au watoto wachache maalumu.

# 3. Simulizi ya Yussuf

Yussuf alizaliwa akiwa haoni. Anaweza kuona mwangaza hafifu tu, lakini hawezi kuona chochote chengine. Hata hivyo, anapenda sana kujituma. Anacheza na ndugu zake na majirani na amekua akijifunza kumsaidia mama yake na baba yake baadhi ya majukumu ya nyumbani. Ana umri wa miaka minne na wazazi wake wanatamani aanze skuli katika umri sawa na watoto wengine, atakapotimiza miaka sita. Wanafahamu kwamba wanapaswa kujipanga sasa kwa kuwa jambo hilo halitokua rahisi.



[Ufafanuzi wa picha: Kuna watoto watatu waliokaa sakafuni ukumbini. Kuna sofa nyuma yao na picha zilizotundikwa ukutani. Mbele yao kuna sufuria mbili zilizobiruliwa. Mtoto wa kiume aliekaa upande wa kushoto akiwa amevaa fulana ya rangi ya manjano amechukua chupa ya plastiki ikiwa na vijiwe vidogo ndani na anaitikisa. Kuna kifimbo cheupe kilicho sakafuni kando yake. Mtoto wa kiume aliyekaa katikati anapiga sufuria na mwiko. Mtoto wa kike aliyekaa upande wa kulia anapiga makofi. Wote wametabasamu na inaonekana wanaburudika.]

Skuli iliopo jirani na anapoishi haipo tayari kumsajili/kumdahili Yussuf. Wanadhani angepaswa kumuandikisha katika skuli maalumu. Lakini skuli ya karibu ipo kilomita 240 kutoka anapoishi, na ina uwezo wa kuandikisha wanafunzi wachache tu kila mwaka. Safari ya kwenda huko ni ndefu na ina gharama kubwa kiasi kwamba Yussuf atalazimika kuonana na familia yake mara mbili tu kwa mwaka. Alihuzunika sana aliposikia hivi na akasema kwamba hataki kabisa kuandikishwa katika skuli hiyo. Wazazi wake wanakubaliana

kwamba ni muhimu Yussuf atumie umri wake wa utoto akiwa na familia na rafiki zake, kwa hivyo wanajitahidi kutafuta ruhusa ya Yussuf kuandikishwa katika skuli jirani.

Skuli inasema kwamba kuna sababu nyingi za kumfanya Yussuf asiweze kuandikishwa katika skuli hiyo. Kwa mfano:

- Skuli haina mwalimu maalumu kwa ajili ya watoto wasioona.
- Walimu wengine hawana uzoefu wa kuwashughulikia watoto wenye ulemavu. Wana hofu.
- Mwalimu mkuu ana wasiwasi kwamba watoto wengine watamfanyia fujo Yussuf.
- Afisa elimu wa Kijiji anasema kwamba ni sera ya serikali kwamba watoto wasioona wanapaswa kuandikishwa katika skuli maalumu.
- Mwalimu Mkuu anasema kwamba skuli haina fedha za kununulia vitabu vya nukta nundu au vifaa vya kuandikia.
- Walimu wanahisi kwamba skuli yao ina mazingira hatari mno kwa mtoto mwenye ulemavu kwa sababu ya ngazi nyingi na mashimo.




[Ufafanuzi wa picha: Wanawake wawili wamesimama wanazungumza, wakiashiria kwa mikono pia. Nyuma yao kuna majengo na bango linalosomeka ‘skuli’. Mwanamke aliyesimama kushoto ameinama kidogo kwa mbele huku akiwa amenyoosha mikono na anaonekana mwenye huzuni. Kando yake kuna mtoto mdogo wa kiume aliyevaa fulana rangi ya njano na miwani myeusi akiwa ameshika fimbo ndefu. Mwanamke anaezungumza nae anaonekana ni mtanashati, mkono wake mmoja akiwa ameshikilia kiuno. Anaonekana amekasirika au mkali akimjibu yule mwanamke mwengine.]

Wazazi wa Yussuf waliemewa na orodha ndefu ya sababu za kumfanya mtoto wao asiandikishwe katika skuli hiyo. Wakahisi hakuna namna zaidi ya kumuandikisha katika skuli maalumu – ndio nafasi pekee kwa Yussuf kusoma.

Siku moja mama yake alikuwa anauza mboga sokoni alipokutana na mteja mpya aliyekuja kununua tungule. Alikuwa haoni lakini mama yake Yussuf alishangazwa na jinsi alivyoweza kwa haraka na usahihi kuhesabu pesa bila ya kuziona. “Natumai mwanangu ipo siku nae ataweza kuhesabu pesa kama unavyoweza wewe”. Hapa ilikua ndio mwanzo wa maongezi. Yule mwanamke asiyeona, Saada, alikua ni mwanachama wa jumuiya ya watu wenye ulemavu, na alisema anaweza kuwapa ushauri wazazi wa Yussuf. Walikubaliana wakutane siku iliyofuata.



[Ufafanuzi wa picha: Kuna wanawake wawili walioelekeana ambao wanazungumza. Baina yao chini kuna aina tofauti za mbogamboga na matunda yanayouzwa. Mwanamke aliye upande wa kushoto amevaa kanzu ndefu na ni mtanashati, ameshika fimbo ndefu nyeupe. Anamkabidhi kitu mwanamke mwengine aliyesimama upande wa kulia ambaye amenyoosha mikono ili kupokea.]

**Miaka miwili baadae Yussuf ameandikishwa katika skuli jirani. Hii iliwezekanaje?**

Saada kwanza aliwasaidia wazazi wa Yussuf kukutana na afisa elimu wilaya (DEO). Alikua mkali, na wazazi wa Yussuf walishaomba kukutana nae mara 3 bila ya mafanikio. Saada alitumia uhusiano alionao na JWU kushinikiza kufanyika kikao cha saa moja. Katika kikao hicho alihadithia uzowefu aliopitia katika maisha yake ya kutafuta elimu (katika mazingira yote, ya skuli maalumu na jumuishi), na alieleza juu ya mikataba ya kimataifa inayosisitiza mifumo ya elimu iwe jumuishi. Hatimaye, afisa elimu wilaya alikubali kwamba Yussuf aandikishwe katika skuli jirani na anapoishi, iwapo Saada ataisaidia skuli kutatua orodha ndefu ya changamoto zilizotajwa. Pia alikubali kuwasilisha ajenda ya kujadili mabadiliko ya sera ya elimu atakapohudhuria kikao kijacho katika Wizara ya Elimu.




[Ufafanuzi wa picha: Kuna watu watano waliokaa katika chumba. Upande wa kulia kuna mwanamme mtanashati aliyekaa nyuma ya meza ambayo juu yake kuna karatasi nyingi. Yupo makini anasikiliza. Mbele yake kuna watu wanne waliomuelekea waliokaa kwenye viti. Karibu kabisa na mtu huyu kuna mwanamke mtanashati aliyevaa kanzu ndefu akiwa ameshika fimbo nyeupe. Anazungumza kwa ishara akielezea jambo fulani. Kando yake kuna kijana mdogo wa kiume aliyevaa fulana rangi ya njano aliyeshika fimbo, na mwanamme mwengine, pamoja na mwanamke ambae alikuwa anauza mbogamboga. Ni wazazi wake].

Hatua nyengine aliyochukua Saada ilikua kuwashawishi baadhi ya walimu kutembelea nyumbani kwa akina Yussuf, kumuangalia Yussuf akicheza na kusaidia kazi za nyumbani. Walipofika, mwalimu mmoja aliuliza "yuko wapi mtoto asiyeona?" walitarajia kumkuta Yussuf akiwa ametulia, bila ya kukimbia huku nah uku akicheza mpira! Baada ya kujionea yote haya walimu wote walikubaliana kwamba Yussuf hakuwa 'asiye na maana' kama walivyotarajia, lakini bado walikuwa na hofu ya kumfundisha.



[Ufafanuzi wa picha:  Watoto walewale watatu wanacheza nje. Mvulana mkubwa yuko upande wa kushoto anaonekana kama anapiga teke. Kuna mpira wa miguu mbele yake. Mvulana mwenye fulana ya njano yupo upande wa kulia anatembea uliko mpira. Mtoto wa kike amekaa mbali upande wa kushoto, anapiga makofi na kumhamasisha. Nyuma yao kuna mtu mzima mwanamme aliyesimama na mwanamke wakitazama na kutabasamu.]

Saada na wenzake katika JWU walishirikiana kwa miezi kadhaa kutafuta jumuiya ambayo ingewapatia baadhi ya walimu mafunzo. Walimu walipatiwa wiki moja ya mfunzo mara tatu katika vipindi tofauti vya likizo. Mafunzo yalijumuisha masuala ya ulemavu na kutumia mbinu za kufundishia zinazomlenga mwanafunzi, na mafunzo hayo yalitolewa na wakufunzi wenye ulemavu na wasio na ulemavu. Walimaliza mafunzo yao miezi 6 kabla ya kuandikishwa kwa Yussuf. Ulipofika muda wa Yussuf kuanza skuli, walimu

walimwambia Saada kwamba walikuwa wanajisikia wanawafundisha watoto wote vizuri zaidi kuliko hapo kabla, kwa hivyo walikuwa wapo tayari kumpokea Yussuf.




[Ufafanuzi wa picha: Kuna watu wazima saba waliokaa kuzunguka meza kubwa wakiwemo wanawake 3 na wanaume 4. Mwanamke mmoja kakalia kitimwendo. Watu wale wale mwanamme na mwanamke kutoka katika picha iliyopita wanaonekana pia katika picha hii. Watu wengine wanazungumza. Mbele yao juu ya meza kuna karatasi kadhaa zenye maandishi na kalamu. Upande wa nyuma wa chumba hicho, kuna mtu anaandika ubaoni. Sehemu ya juu ya ubao kuna maneno yanayosomeka ‘Mafunzo ya Elimu Jumuishi kwa walimu, Siku ya Pili’.]

Baada ya Yussuf kuandikishwa, mwalimu wake wa darasa alishirikiana na Saada, Yussuf pamoja na wazazi wake kuandaa orodha ya shabaha zao za awali. Hii ilijumuisha vitu gani Yussuf aanze kujifunza, jinsi gani mwalimu atamsaidia, na usaidizi gani wa ziada ambao mwalimu atauhitaji kutoka kwa wenzake, Saada, wazazi au watu wengine.

Skuli ilikua haimudu kumuajiri mwalimu maalumu, na wazazi wake Yussuf walikuwa na hofu kwamba nani angeweza kumfundisha mtoto wao ujuzi kama vile wa kusoma nukta nundu na kuandika. Baada ya utafiti wa muda, Saada

aliwaalika vijana wawili wasioona kutoka katika Kijiji chengine, kumtembelea Yussuf mara mbili kwa wiki, ili kumfundisha misingi ya kusoma na kuandika nukta nundu. Vijana hawa walikuwa wamemaliza mafunzo katika skuli maalumu lakini walikuwa hawajaajiriwa. Walikua tayari kujitolea iwapo mama yake Yussuf angewapatia chakula cha mchana. Mmoja kati ya vijana hawa aliweza kuishawishi skuli aliyosoma kuchangia ubao wa nukta nundu na kalamu ya kuandikia nukta nundu kwa ajili ya Yussuf. Kijana mwengine wa kujitolea alifurahia sana kumsaidia Yussuf kiasi kwamba – kwa msaada wa JWU – alitunukiwa fursa ya ufadhili wa kwenda kusomea ualimu, mwakani. Anakusudia kufanya mafunzo yake ya vitendo katika skuli ya akina Yussuf akitumai siku moja awe muajiriwa kamili wa skuli.



[Ufafanuzi wa picha: Kuna wanafunzi darasani. Wamekaa kwenye meza wakifanya kazi katika jozi. Kwenye dawati lililopo mbele upande wa kushoto mtoto wa kiume asiyeona anatumia ubao wa nukta nundu na kalamu yake. Karibu yake kuna kijana wa kiume ameinamia upande wake akimsaidia. Upande wa kulia kuna kijana wa kike anaemsaidia mwanafunzi mwengine. Upande wa nyuma mtu yuleyule aliyeonekana katika picha mbili zilizotangulia anaangalia huku akitabasamu.]

Walimu waliamua kuwatayarisha watoto wengine kumpokea Yussuf atakapofika skuli, kwa hivyo waliandaa shughuli mbalimbali kuwafundisha

watoto kuhusu ulemavu na haki za watoto. Watoto walifahamu haraka sana na wakaanza kuuliza iwapo wangeweza kufanya marekebisho yoyote kuifanya skuli iwe salama kwa Yussuf atakapowasili. Walitumia muda wao wa mapumziko kuokota mawe kujaza katika uwanja wa kuchezea ili uwe tambarare na salama. Pia walitumia mawe kuweka alama za njia kutoka getini kuelekea darasani na maktaba. Watatu kati yao walikubaliana kumuonesha Yussuf njia hizi siku ya mwanzo atakapowasili. Baadhi ya watoto walikwenda kuzungumza na wazazi wao nyumbani.




[Ufafanuzi wa picha: Kuna watu wengi, wanaume, wanawake na watoto wakishirikiana pamoja kufanya kazi mbele ya skuli. Kuna mtu mmoja mwanamme anasukuma mkokoteni/ tolorilililobeba mawe. Baadhi ya watu wanapanga mawe kutengeneza kingo za njia zinazoelekea skuli. Mtoto mmoja wa kiume aliyekaa kwenye kitimwendo anaashiria mahali pa kupanga mawe. Kwa nyuma mwanamke mtanashati aliyevaa kanzu ndefu anazungumza na mwanamke mwengine mtanashati (mwalimu mkuu). Mtoto wa kiume aliyevaa fulana rangi ya njano anatembea ubavuni mwa mama yake ambae amechukua chupa za maji ya kunywa.]

# 4. Tunawezaje kushirikiana kuisaidia skuli kuwa jumuishi zaidi?

**Ushirikiano ndio moyo wa mafanikio katika elimu mjumuisho.** Kwa mfano, asasi zisizo za kiserikali zinaweza kuwa na uzoefu zaidi katika kuhamasisha mabadiliko ya kimfumo kama vile sera, wakati jumuiya za watu wenye ulemavu zina nafasi nzuri ya kushughulikia mahitaji ya mtu mmoja mmoja, kama vile huduma za marekebisho au vifaa. Lakini zikifanya kazi bila ya ushirikiano, kila taasisi itakua inatoa sehemu ndogo ya ufumbuzi huku kukiwa na nafasi finyu ya kufanikiwa.

Unakabiliwa na vikwazo gani katika jamii yako katika jitihada za kuhakikisha wanafunzi wote **wanahudhuria** skuli, **wanashiriki** katika mchakato wa kujifunza, na **wanafikia** ukomo wa uwezo wao wa kujifunza?

- Tunawezaje kuondoa vikwazo hivyo? Hatua gani zichukuliwe?
- Nani anapaswa kujumuishwa katika kuchagua, kuendeleza na kutekeleza hatua za ufumbuzi? Kila mtu anapaswa kufanya nini?
- Kwa namna gani kufanya kazi kama timu kunatoa njia muafaka ya kuondoa kikwazo hiki ukilinganisha na kila mtu kutafuta ufumbuzi peke yake?





Mfano wa mkeka wa uchambuzi wa vikwazo kutoka Zanzibar

[Ufafanuzi wa picha: Karatasi kubwa imebandikwa ukutani, imegawanywa katika mistari wima minne yenye kichwa cha habari ‘vikwazo’, ‘vipi’, ‘nani’, ‘nini’. Majibu yameandikwa chini ya kila kichwa cha habari.]

# 5. Kufahamu mahusiano ya kimadaraka

Kuna vyanzo tofauti vya madaraka au sababu katika maisha zinazowawezesha watu kuwa na madaraka, ambapo sisi kama mtu mmoja mmoja hupata madaraka hii kwa kujua au kutokujua. Kwa mfano:




Flipchati iliyokusanya mawazo ya mjadala kuhusu nani mwenye madaraka katika skuli ya kijijini

[Ufafanuzi wa picha: Kuna flipchati yenye duara kubwa lenye neno ‘mwenye madaraka zaidi’ lililoandikwa katikati ya duara hilo. Kuna vikaratasi vya rangi ya waridi vyenye maandishi kuhusu mgawanyo wa majukumu kama vile ‘viongozi wa dini’, ‘mhadhiri wa chuo kikuu’, ‘polisi’, na kadhalika vilivyobandikwa katika maeneo tofauti ndani na nje ya duara.]

## Madaraka yanaweza pia kuwa ya mtu binafsi au ya kikundi cha watu, kama inavyooneshwa na tafsiri zifuatazo:

“Madaraka ni uwezo wa kutekeleza **malengo binafsi** na kuwashawishi wengine kufikia malengo hayo. Ni uwezo wa kupata tunachokitaka, kuhodhi tulichonacho, na kusawiri matukio katika namna tunayotaka yawe.”

“Kwa **ngazi ya kikundi**, madaraka ni uwezo wa kuunganisha vyanzo tofauti vya madaraka ya mtu mmoja mmoja ili kuleta mabadiliko tunayoyatamani ambayo hunufaisha kikundi badala ya mtu mmoja mmoja.”

**Madaraka yanaweza kugawiwa katika makundi yafuatayo:**

**Madaraka/nguvu dhidi:** falsafa hii inaamini kwamba madaraka ni kitu maalumu – mtu mmoja ama kikundi kinapopata madaraka zaidi, wengine hupunguziwa.

**Madaraka/nguvu kwa:** aina hii ya madaraka yanayoelezea aina fulani ya uwezeshaji. Inamuwezesha mtu kudhibiti au kusimamia hali fulani kwa manufaa yake.

**Madaraka/nguvu pamoja na:** hii inajumuisha madaraka ya pamoja na huonekana pale kikundi kinapotatua changamoto pamoja, na kutengeneza madaraka ambayo ni makubwa kuliko jumla ya madaraka ya watu wanaounda kikundi hicho.

**Madaraka/nguvu ndani ya:** madaraka yanaishi ndani ya mtu na kuwakilisha madaraka ya ndani. Inatokana na kujikubali na kujiheshimu, ambayo nayo hutokana na kuwaheshimu wengine na kukubali kwamba watu wote ni sawa.

- 'Madaraka/nguvu dhidi' ni mtazamo ambao mara nyingi tunautumia kuonea madaraka.
- Tunachukulia kwamba iwapo mtu mmoja/kikundi katika uwiano ana madaraka zaidi, waliobaki katika uwiano huo lazima wawe hawana madaraka. Tunachukulia kwamba iwapo asiye na madaraka (dhaifu) atapata madaraka mpya, aliye na madaraka zaidi lazima apoteze sehemu ya madaraka zake, kwa sababu kuna kiwango kidogo sana cha madaraka ambazo watu wanaweza kushirikiana pamoja!
- Muwezeshaji wa Shirikisho katika ngazi ya Wilaya akifanya igizo kuhusu 'ushirikiano wenye ufanisi' mjini Kampala, Uganda
- Hii huonekana katika mijadala ya jinsia, ambapo wanaume huhofia mwanamke kuwa na madaraka kwa sababu ya athari hasi ambayo wanadhani itawakumba. Jamii inaamini kwamba usawa wa jinsia unamaanisha kwamba wanaume watalazimika kusalimisha sehemu ya madaraka yao kwa wanawake na kwa kufanya hivyo wanaume watapoteza nafasi na hadhi yao
- Mtazamo huu wa mahusiano ya kimadaraka ambapo upande mmoja unaweza tu kupata madaraka iwapo upande mwengine utapoteza hautotusaidia sisi kufikia lengo la jamii changamano na isiyo na ubaguzi.

Kufikia malengo yetu tunahitaji kubadilisha namna ambavyo sisi (na wengine) tunavyoifahamu madaraka. Hii inamaanisha kutafuta namna ya kurahisisha katika kazi zetu uwepo wa 'madaraka ndani ya' na 'madaraka kwa' – na kuifahamu zaidi madaraka kama rasilimali isiyo na mipaka – bali kuna madaraka ya kumtosheleza kila mtu!



[Ufafanuzi wa picha: picha inamuonesha mwanamke mmoja akiwa amepiga magoti kwenye sakafu mbele ya mwanamke aliyekaa kwenye kiti na mwanamme aliyekaa kwenye kitimwendo. Kuna viti vyengine vilivyowazunguka. Wanazungumza na kuashiria.]

Kufanya kazi kwa ushirikiano kama sehemu ya kikundi au timu kunaweza kuwa na changamoto mpaka pale **kila mwanakikundi au timu atakapoonekana ni sawa na mwengine** na kufahamika kwamba **kila** mwanakikundi ana mchango tofauti wa kuimarisha, elimu na uzoefu ambao utasaidia katika kufikia malengo ya elimu jumuishi. Hii inaakisi uhalisia kwa jumuiya za watu wenye ulemavu na Shirikisho katika ngazi ya Wilaya na pia tunapoanzisha na kusimamia kamati za elimu mjumuisho za skuli.

Kamati ya elimu mjumuisho ya skuli inaweza kuwa na mratibu lakini akawa **hana** madaraka ukilinganisha na wajumbe wengine wa kamati. Kamati ya elimu mjuisho ya skuli haiwezi kufanikiwa iwapo itatumika kama chombo cha mtu binafsi cha kujiimarisha.

## Kuhaulisha mahusiano ya kimadaraka

**Picha ya 1: Madaraka dhidi**
Picha hii inamuonesha mwanamke mtanashati, ambaye huenda ni mwalimu mkuu akionekana kama kwamba anakataa kuandikishwa skuli mtoto asiyeona. Mama wa mtoto anazungumza na mwalimu mkuu, inaonekana kama kwamba anamuomba aruhusu mwanawe kuandikishwa katika skuli hiyo lakini hana madaraka ya kumshawishi kwa jinsi hali ilivyo. Fikra ni kwamba mwalimu mkuu ana madaraka dhidi ya mama wa mtoto mwenye ulemavu. Mwalimu mkuu anaweza pia kujihisi ana udhaifu fulani akihisi kwamba skuli yake haina mazingira wezeshi kwa mtoto.





[Ufafanuzi wa picha: Wanawake wawili wamesimama wanazungumza, wakiashiria kwa mikono. Nyuma yao kuna majengo na bango linalosomeka ‘skuli’. Mwanamke aliyesimama kushoto amevaa mavazi yake yaleyale ya kila siku, na ameinama kidogo kwa mbele huku akiwa amenyoosha mikono na anaonekana mwenye huzuni. Kando yake kuna mtoto mdogo wa kiume aliyevaa fulana rangi ya njano na miwani myeusi akiwa ameshika fimbo ndefu. Mwanamke anaezungumza nae amevaa kwa umaridadi mkono wake mmoja akiwa ameshikilia kiuno. Anaonekana amekasirika au mkali akimjibu yule mwanamke mwengine.]

**Picha ya 2: Madaraka na**
Picha hii inamuonesha mama wa mtoto asiyeona akiwa kwenye kikao na kamati ya ujumuishi ya skuli (SIT) kujadili jambo fulani. Anasikilizwa na wajumbe wa kamati na huwenda anahisi anaungwa mkono na wanaomsikiliza na kwamba hayupo peke yake katika changamoto inayomkabili. Mwanawe pia yupo kwenye kikao. Inaonesha kwamba anajisikia ana madaraka na kamati inayomsikiliza, madaraka ya pamoja kwa kutatua changamoto pamoja.



[Ufafanuzi wa picha: Kuna watu 9 waliokaa katika umbo la nusu duara katika mabenchi katika chumba chenye madirisha matatu nyuma. Kupitia kwenye madirisha unaona majengo ambayo yanafanana na skuli. Miongoni mwa waliokuwepo katika kikundi ni mwanamme aliyekaa kwenye kitimwendo, mzee mmoja akiwa ameshika fimbo ya kutembelea na mtoto wa kike aliyevaa sare za skuli akiwa na mguu mmoja na gongo la kutembelea, na wanawake wengine watatu na mwanamme mmoja. Mwanamke yuleyule ambae huvaa nguo zile zile kila siku nae pia yupo katika kikao anazungumza. Kando yake, aliyekaa kwenye benchi ni mtoto mdogo wa kiumealiyevaa miwani myeusi akiwa ameshika fimbo ndefu. Watu wote wanamsikiliza yule mwanamke na nyuso zao zinaonesha kuguswa mno.]

**Picha ya 3: Madaraka ndani ya**
Picha inamuonesha mama wa mtoto asiyeona akiwa amesimama nje ya skuli anazungumza na wadau mbali mbali wa skuli. Kuna watu wengi waliokaa wakimsikiliza. Mwanawe yupo kando yake, akiwa ameshika mkono wa mtu, anaeonekana kuwa ni baba yake. Uwepo wa baba yake unaonesha kwamba anashirikiana kwa karibu na mkewe. Mwalimu mkuu amejumuika na wajumbe wengine kumsikiliza mama wa mtoto asiyeona. Inaonesha kwamba mama wa mtoto anajisikia kuwa na madaraka ndani yake na hata lugha yake ya ishara ni tofauti na mara ya mwanzo alipokutana peke yake na mwalimu mkuu, anaonekana amewezeshwa na mwenye kujiamini.




[Ufafanuzi wa picha: Kuna kundi kubwa la watu 20 au 30 wakiwa wamekusanyika kwenye viti, nje ya skuli. Mwanamke aliyevaa mavazi ambayo huvaa kila siku amesimama akiuhutubia mkusanyiko. Kando yake kuna mwanamme aliyesimama akiwa amevaa shati na suruali, akiwa ameshika mkono wa mtoto yule yule aliyevaa sare za skuli huku ameshika fimbo ndefu. Watu waliokaa kwenye viti wanamsikiliza kwa umakini mwanamke anayezungumza. Miongoni mwao, aliyekaa mstari wa mbele, ni mwanamke mtanashati, anayesikiliza. Anaonekana mwenye kukubaliana na kinachozungumzwa. Pia kuna watu wengine ambao si wapya kama vile mwanamme aliyekaa kwenye kitimwendo, mzee mwenye fimbo ya kutembelea (mkongojo), mwanamke aliyevaa hijabu na mtoto wa kike mwenye mguu mmoja.]

# 6. Ushirikiano na kamati ya elimu mjumuisho ya skuli

Wazazi na jamii mara nyingi huwa hawashirikishwi katika sekta ya elimu na inawezekana wakawa hawajui huduma zinazotolewa, na msaada na elimu wanayoweza kuitoa.

Walimu wengi na waelimishaji wengine hufanya kazi peke yao na hukabiliana na changamoto katika kukidhi mahitaji ya wanafunzi wote wanaowashughulikia. Wakati mwengine hufanya kazi kwa bidii lakini hukosa uungwaji mkono, fursa za mafunzo na vitendea kazi vya kuwasaidia kuwa jumuishi zaidi.

Kwa ufupi, mara nyingi kuna **ukosefu wa ushirikiano,** ambao ni lazima uwepo iwapo skuli na jamii inahitaji kuwa jumuishi.

Kumbuka, ijapokuwa wewe sio sehemu ya wajumbe wa kamati ya elimu mjumuisho ya skuli (SIT) **una jukumu kama mwanachama wa JWU, mzazi au mwanajamii kusaidia na kushirikiana na SIT** ili kuisaidia skuli yako iwe jumuishi zaidi.

## Kwa namna gani JWU inaweza kuchangia katika kamati ya elimu mjumuisho ya skuli?

- Kuna fursa zipi za kukuwezesha kushirikiana na kuzisaidia Kamati ya elimu mjumuisho katika wilaya yako?
- Kuna vikwazo vipi maalumu kwa elimu mjumuisho ambavyo unadhani Shirikisho lenu katika nagazi ya Wilaya linaweza kusaidia kuviondoa?
- Kwa namna gani Shirikisho lenu linaweza kuisaidia SIT kuwa endelevu hata baada ya muda wa utekelezaji wa mradi kwisha?

# 7. Jukumu la mratibu wa elimu mujumuisho wa skuli (IECo)



Mratibu wa elimu mjumuisho wa skuli (IECo) ni nafasi ya kujitolea.

Mratibu wa elimu mjumuisho anapaswa kufanya kazi ya uratibu; hii inamaanisha kuandaa na kuendesha mikutano na kufuatilia utekelezaji, badala ya kuwa na wajibu kamili wa kufanya utambuzi, tathmini na kutoa elimu mjumuisho.

Anapaswa kuwa mjumbe wa kamati ya skuli ya elimu mjumuisho na asaidie kufikia malengo ya mwenendo wa ujumuishi, sera na utekelezaji katika skuli.

Mratibu wa elimu mjumuisho ataandaa mikutano ya pamoja ya skuli mbalimbali, vitongoji na jamii akizihamasisha kuongoza harakati za elimu mjumuisho na kujivunia mabadiliko katika skuli zao.

Mratibu wa elimu mjumuisho ni mtu muhimu anaepaswa kuhakikisha kwamba watoto wote wana haki ya kupata fursa za kujifunza na kufikia ukomo wa vipaji vyao.

Yeye ndiye kiunganishi kikuu baina ya wanafunzi, familia, jamii, skuli na wataalamu wengine ambao wanaunda mtandao wa usaidizi kwa skuli na jamii jumuishi.


# Mratibu wa elimu mjumuisho (IECo) anafanya kazi katika viwango tofauti




# Shughuli ambazo mratibu wa elimu mjumuisho wa skuli anaweza kushiriki katika ngazi ya skuli, jamii na wizara

## Skuli

- Kuujengea uwezo na kuuhamasisha uongozi wa skuli, walimu na wafanyakazi wengine;
- Kuhakikisha kwamba mipango ya skuli ni jumuishi;
- Kutathmini miundombinu kuona iwapo inakidhi vigezo vya ufikiwaji;
- Ushauri juu ya kutengeneza aina fulani ya vitendea kazi;
- Mafunzo kuhusu mbinu za darasa jumuishi;
- Kuimarisha ushirikiano baina ya skuli na jamii;
- Kuwafuatilia na kuwatathmini wanafunzi mmoja mmoja;
- Kuandaa majadiliano ya vikundi kwa walimu na wanafunzi;
- Kupendekeza shughuli kwa mkabala wa ujumuishaji wa skuli nzima;







## Kwenye jamii

- Kukuza uelewa katika ngazi ya jamii;
- Kujenga ushirikiano baina ya skuli na jamii;
- Kutembelea mwanafunzi mmoja mmoja nyumbani kwao inapolazimu;
- Kuhudhuria vikao vya Kijiji;
- Kuandaa rufaa kwa huduma zinazopatikana kijijini – kwa mfano, huduma za uchunguzi wa afya katika skuli;
- Kubaini ujuzi na vifaa vinavyopatikana kijijini ambavyo vinaweza kutumika skuli – kwa ajili ya kufundishia, n.k.
- Kuwafundisha watendaji wa kujitolea wa Kijiji mbinu za kuwabaini wanafunzi;
- Kuandaa mafunzo ya mtaalamu kwa ajili ya wazazi/walezi yatakapohitajika.

## Na wizara ya Elimu/katika ngazi ya sera

- Kuhudhuria vikao vya baraza kwa lengo la kukuza uelewa na kuhoji kuhusu fursa za ufadhili;
- Kukuza uelewa kupitia vyomba vya habari – redio ya kijiji na magazeti;
- Kuhudhuria vikao vya mipango ili kuhakikisha kwamba mipango yote ni jumuishi;
- Kuzishirikisha NGOs na asasi za kijamii katika mafunzo yoyote kuhusu elimu jumuishi katika vituo vya elimu au maeneo mengine muafaka;



## 8. Fursa za ushirikiano katika jamii zetu

Kujenga mtandao madhubuti wa uungaji mkono elimu mjumuisho ni muhimu sana kwa skuli na kamati zake za ujumuishi. JWU zina jukumu muhimu katika kujenga na kuendeleza mitandao hii. Ili kujenga mtandao imara tunahitaji KUANGALIA aina gani ya usaidizi inayopatikana katika jamii na KUTAFAKARI juu ya namna gani tunaweza kuunda uhusiano thabiti wa ushirikiano kwa ajili ya elimu jumuishi katika jamii nzima.

Ijapokuwa ni muhimu kuvitambua vikwazo vinavyokabili elimu mjumuisho katika jamii zetu, ni muhimu pia kutambua kwamba kuna mambo mengi mazuri yaliyopo katika jamii zetu ambayo tunaweza kuyatumia kusaidia elimu mjumuisho.

Tunaweza kuyachukulia mambo haya mazuri kama madaraka tuliyonayo ambayo itatusaidia kuvunja vikwazo na kuimarisha uwezo wa skuli kwa ajili ya elimu mjumuisho. Madaraka hizi zinaweza kuchkuliwa kama rasilimali au kitu cha thamani katika jamii.

# Tunaona nini tunapoiangalia jamii yetu?

## Unapoziangalia hizi picha tatu katika kurasa tatu zifuatazo, unaona nini?



[Ufafanuzi wa picha: Kuna kijana anayeonekana katikati ya picha. Kando yake kuna punda wawili na yeye ameinama na kushikilia mguu mmoja wa mbele wa mmoja kati ya punda hao. Nyuma ya kijana huyo kuna punda mwengine ambaye amefungwa kwenye mkokoteni wenye magurudumu mawili. Kuna pipa la bluu lililofungwa kwenye mkokoteni. Pia kunaonekana katika picha hii mwanamke ambaye anatembea karibu na mkokoteni. Nyuma ya picha kuna jengo dogo lililoharibika. Haijulikani jengo hilo ni nini, lakini kwenye moja ya kuta zake, kumeandikwa maneno "Imefadhiliwa na Tume ya Ulaya". Mbele ya jengo hilo kumeegeshwa gari kubwa jeupe. Eneo la mbele ya jengo ambalo kijana ameinama na mwanamke anatembea, kuna mchanga mkavu, mgumu na mawe mengi juu yake. Pia kuna takataka nyingi chini, hasa chupa za plastiki na vifungashio mbalimbali]']



[Ufafanuzi wa picha: Katika picha hii kuna sehemu ya mchanga yenye miamba mikubwa mingi. Kuna jengo kubwa la zege la kijivujivu nyuma. Chini yake kuna mahema makubwa meupe. Katikati ya picha kuna hema kubwa zaidi. Vipande vya hema vya hema hili viko wazi na unaweza kuona baadhi ya watu wameketi kwenye hema wakizungumza. Mbele ya hema kuna mtoto mdogo wa kiume anayeendesha baiskeli ndogo. Karibu na hema hilo kuna mifuko mingi myeupe. Pia kuna sehemu ya kufulia nguo katikati ya mahema mawili na pia kuna nguo zilizoanikwa juu ya kamba.]



[Ufafanuzi wa picha: Katika picha hii kuna kibanda kikubwa kilichotengenezwa kwa vipande vya mabati ambavyo vimeunganishwa. Kuna michoro ya picha katika baadhi ya sehemu za kibanda. Kuna mtu mmoja ameketi kwenye sanduku jeupe la plastiki, nje kidogo ya kibanda hicho. Karibu na mtu huyo kuna dumu kubwa kubebea maji lenye rangi ya njano. Kuna takataka nyingi - mirija ya plastiki, mifuko mikubwa myeupe iliyorundikana, makopo matupu na pia kuna kitu kinachoonekana kuwa ni godoro bovu na chafu sana. Nyuma ya kibanda hicho kuna rundo kubwa la takataka. Kuna mtu amesimama kwenye rundo la takataka akilitazama na kuna mtu mwengine amesimama akitazama rundo hilo la takataka. Kwa nyuma pia kuna gari kubwa karibu na jaa.]

## Tunapotazama hizo picha tatu, je, tunaona mambo yaliyo hasi tu au tunaweza kuona mambo yaliyo chanya pia?

# 9. Kutoka matatizo hadi rasilimali

Ingawa ni muhimu kuangalia matatizo kila mara au kuangalia yale yasiyo sahihi katika jamii na kuelewa ni kwa namna gani haya yanaweza kuwa ni vikwazo vya elimu mjumuisho, kwa mfano, umaskini, ni muhimu pia kutafakari juu ya mambo katika jamii yanayoweza kusaidia kuondoa vikwazo hivi na kuimarisha uwezo wa skuli kwa ajili ya elimu mjumuisho.

Tunaweza kuona mambo haya mazuri kama uimara au kitu cha thamani ndani ya jamii - tunaweza kuziita **RASILIMALI**.

Raslimali katika jamii zinaweza kusaidia kuondoa vikwazo vya elimu mjumuisho au zinaweza kusaidia kuleta mabadiliko.

Tunaweza kutumia rasilimali katika jamii kusaidia Kamati ya elimu mjumuisho na kusaidia kuongeza uwelewa kuhusu elimu mjumuisho.

Angalia **picha ya wanajamii** iliyopo ukurasa unaofuata:

- Je, ni rasilimali gani unaweza kuziona kwenye picha ambayo inaweza kuwa muhimu kama usaidizi au nyenzo kwa Kamati ya elimu mjumuisho?
- Je, rasilimali hizi zingewezaje kusaidia kukabiliana na vikwazo vya elimu mjumuisho ambavyo walivitambua na vilijadiliwa siku iliyopita?
- Je, rasilimali hizi zinawezaje kuwa msaada au nyenzo kwa Kamati ya elimu mjumuisho?


DUKA LA KUSHONA NGUO
MGAHAWA
SOKO

[Ufafanuzi wa picha. Picha inaonesha sehemu ya jamii. Upande wa juu kushoto kutoka nyuma kabisa kuna kanisa dogo na nje ya kanisa kuna kikundi cha watu wakiwa wamesimama wanaimba. Mbele yao kuna mtu anayeongoza kwaya. Kanisa lipo kwenye mteremko wa mlima na masafa mafupi upande wake wa kulia kuna watoto wawili wa kiume wakifukuzana. Pia kwenye mteremko wa mlima upande wa kulia wa picha kuna jengo lenye madirisha mengi na mnara mkubwa wa saa katikati. Nje ya jengo kuna bango linalosomeka "Chuo Kikuu" na mbele ya bango kuna watu watatu. Vijana wawili wanazungumza na mmoja wao kabeba begi mgongoni. Hatua chache mbele yao kuna mtu anaetoka nje ya jengo akiwa amechukua faili.]

Karibu na katikati ya picha kuna jengo dogo lililoezekwa kwa bati. Lina milango miwili mikubwa iliyo wazi, kwa ndani anaonekana mtu aliyekaa kwenye kitimwendo, akiwa mbele ya meza yenye skrini ya kompyuta. Kando yake kuna mashine ya kurudufu (kutolea fotokopi). Pia ndani ya jengo hilo hilo kuna mtu ambae anampiga picha mtu mwengine aliyesimama mbele yake. Nje ya jengo upande wa kushoto kuna mtu anaetembea kando yake, na upande mwengine kuna kibanda chenye mbwa wawili wanaocheza.

Hatua chache kutoka kwenye kibanda kuna mtu aliyesimama chini ya kibanda kilichotengenezwa kwa bati. Kwenye kibanda kuna vitanda vilivyopangwa katika mistari miwili. Mbele ya kibanda kuna dereva wa bodaboda anaepita akiwa amepakia mizigo miwili mikubwa nyuma. Karibu na dereva wa bodaboda kuna mtu anaekata barabara akiwa kashika fimbo.

Mbele ya picha upande wa kulia kuna jengo jengine dogo lililoezekwa kwa bati. Milango ya jengo hili imefunguliwa na ndani kuna wanawake watatu. Kwenye kuta za jengo kumeegemezwa marundo ya vifaa vyenye rangi tofauti. Wawili kati ya wanawake waliopo wamesimama pamoja. Mmoja amenyoosha mikono na mwengine amesimama nyuma yake akimpima mikono yake. Kando yao kuna mwanamke mwengine aliyekaa kwenye meza ndogo yenye cherehani.


Nje ya jengo hili kuna wanawake wawili wliokaa chini wakiuza matunda na mbogamboga. Kila muuzaji yupo kando ya kipolo cheupe kilichotandikwa chini. Muuzaji wa kwanza ana viche vya mbogamboga vilivyopangwa kwa umaridadi juu ya kipolo cheupe. Pia ana mimea myengine midogo midogo iliyopo kando ya kipolo na ameinama akiishika mimea hiyo. Mbele yake kuna kijana wa kike aliyechukua kikapu kidogo huku amebeba mtoto mgongoni. Muuzaji mwengine amekaa juu ya kipolo akiwa na mafungu ya matunda mekundu yaliyopangwa vyema mbele yake. Anazungumza na kijana wa kiume mwenye gongo la kutembelea ambae anaangalia matunda.]

# Kuna rasilimali gani?

Rasilimali inaweza kuwa ni ujuzi vitendo (mf. Ufundi seremala)




Picha ya 1: Kuna kibanda kidogo kilichotengenewa kwa mabati na kuna fremu za mbao za vitanda 10 chini ya kibanda hicho vilivyopangwa katika mistari miwili. Kuna mtu mmoja katika kibanda hicho akitengeneza kimoja kati ya vitanda hivyo.]




Rasilimali inaweza kuwa maarifa fulani aliyonayo mtu (mf. maarifa ya mhadhiri wa chuo kikuu)

Picha ya 2: Kuna jengo lenye madirisha mengi na mnara mkubwa wa saa katikati. Nje ya jengo kuna bango linalosomeka “Chuo Kikuu” na mbele ya bango kuna watu watatu. Vijana wawili wanazungumza na mzee aliyevalia vizuri, akiwa amechukua vitabu.

Rasilimali anaweza kuwa mtu mwenye ushawishi katika jamii, kama vile imamu.




[Pichay a 3: kuna msikiti. Nje ya msikiti kuna wanaume watatu wamesimama pamoja wanazungumza. Mwanamume mmoja ana gongo la kutembelea. Mmoja wapo wa watu hao ni imamu wa msikiti]




Rasilimali zinaweza kuwa ni nyenzo halisi katika jamii (mf. ukumbi wa kanisa au mkahawa ambapo watu wanaweza kukutana)

Picha ya 4: Kuna kibanda cha miti kilichoezekwa kwa mabati. Mlango mmoja wa kuingilia kibandani umefunguliwa na ndani kuna sufuria inayochemka. Nje ya kibanda kuna watu wamekaa kwenye meza mbili ndogo. Katika meza moja kuna mtu mzima wa makamo na kijana wa kike. Kila mmoja ana chupa mbele yake na wanazungumza. Kando yao kuna kijana wa kiume akiwa amekaa peke yake kwenye meza na ana sahani ya chakula mbele yake. Nyuma ya kijana huyu kuna birika inayochemka jikoni.]

Rasilimali inaweza kuwa jumuiya inayofanya kazi zake katika jamii (kwa mfano jumuiya ya wanawake)




Picha ya 5: kuna kikundi cha wanawake wamekaa nusu mduara katika viti.


Ingawa rasilimali nyingi ziko wazi kwetu, wakati mwingine haziko wazi, na tunahitaji kufikiria jinsi mtu au kitu kinavyoweza kuwa rasilimali inayoweza kutumika baadae.

# 10. Jinsi ya kutengeneza ramani ya rasilimali za jamii

- Ramani ya rasilimali ya jumuiya ni kama ramani ya mawazo ya jumuiya.
- Inaonesha WATU, NYENZO na JUMUIYA mbalimbali ambazo zinaweza kuwa rasilimali tarajiwa na msaada wanaoweza kutoa.
- Inaonesha pia jinsi mali hizi zinavyoweza kuunganishwa ili kuunda mtandao unaoweza kusaidia Kamati ya elimu mjumuisho na kuimarisha usaidizi wa jamii kwa elimu mjumuisho.
- Fikiria kuhusu mifano maalum katika jamii/wilaya yako ya watu, nyenzo na jumuiya ambazo zingeweza kuwa rasilimali.
- Jadili jinsi wanavyoweza kuzisaidia Kamati ya elimu mjumuisho na kuchangia katika maendeleo ya Elimu Mjumuisho.
- Kwa jinsi ulivyotengeneza ramani ya mawazo yako, jadili namna ambavyo ungependa kuwasilisha rasilimali ya jumuiya yako kama ramani
- Chora ramani yako (angalia mfano wa ramani hiyo katika ukurasa unaofuata)

Mifano ya aina za mali zinazopatikana katika jamii

| | |
|---|---|
| **Watu** | · Mtu mwenye maarifa ya mambo muhimu<br>· Mtu mwenye ujuzi tunaoweza kuutumia<br>· Mtu mwenye uzoefu unaoweza kutusaidia<br>· Mtu anaeweza kujitolea kwa muda<br>· Mtu mwenye jukumu la uongozi na anaweza kutumia nafasi yake kusaidia katika elimu mjumuisho |
| **Rasilimali vitu** | · Sehemu tunayoweza kuitumia kufanyia mikutano<br>· Huduma ya kiserikali ambazo kamati ya skuli ya elimu mjumuisho inahitaji kuisaidia<br>· Msikiti unaowaleta wanajamii pamoja<br>· Aina mbalimbali za usafiri wa umma<br>· Maduka yanayoweza kutoa rasilimali kwa skuli |
| **Jumuiya zisizo za kiserikali** | · Jumuiya inayotoa huduma ambayo kamati ya skuli ya elimu mjumuisho inaweza kutumia<br>· Jumuiya inayoweza kusaidia kufikia jamii flani<br>· Jumuiya inayoweza kusaidia kukuza uelewa na kusambaza tarifa |



Bwana P Mwalimu Mstaafu
(husaidia kuzungumza na wazazi)
Bwana K fundi Cherehani
Skuli
Soko la mboga mboga
(Mimea ya skuli)
Chuo Kikuu
Imamu Msikitini
Watu
Rasilimali Vitu
Dereva wa Bodaboda
(Usafiri)
Bwana C mmiliki wa mgahawa (Vikao)
Ardhi
Mto
Taasisi
Jumuiya za madereva wa bodaboda
Jumuiya za wanawake
Makundi ya Vijana
(wanasaidia kugawa vitini)

[Ufafanuzi wa picha: Katikati ya kipande cha karatasi kuna maduara matatu yaliochorwa kwa mkono yaliyopangwa katika umbo la pembe tatu. Katika duara la kwanza upande wa kushoto pameandikwa neno “watu”. Duara jengine limeandikwa “jumuiya” na la tatu lina maneno “rasilimali zinazoonekana”. Maduara matatu yameunganishwa pamoja kwa mistari myeusi.]

Katika mzunguko wa duara la “watu” kuna maduara madogo madogo manne yote yameunganishwa na duara hilo kwa mstari mweusi. Katika moja kati ya maduara haya madogo kuna kikongwe aliyeshika fimbo na chini yake pameandikwa ndani ya duara “Bw. P. mwalimu mstaafu” na chini ya maneno haya katika mabano pameandikwa “husaidia kuzungumza na wazazi”. Duara jengine katika maduara madogo kuna picha ya kijana wa kike akiwa amekaa anashona kwa kutumia cherehani na chini yake pameandikwa “Mama K. mshoni”. Duara jengine dogo lina maneno “Imam msikitini”. Katika duara jengine dogo kuzunguka duara la watu kuna picha ndogo ya kibanda kilichoezekwa bati. Nje ya kibanda kuna watu waliokaa kwenye meza. Wawili wanazungumza na mwengine amekaa anakula. Kuna birika nyuma yake inachemka jikoni.


Kuzunguka duara la “jumuiya” kuna maduara madogo matatu yaliounganishwa na duara hilo kwa mstari mweusi. Duara dogo la mwanzo lina picha ya dereva wa bodaboda na chini yake pameandikwa “Chama cha madereva wa bodaboda”. Duara jengine dogo lina picha ya kikundi cha watu waliokaa wanazungumza. Chini ya picha pameandikwa “Kikundi cha Vijana” na kwenye mabano pameandikwa “husaidia kusambaza machapisho”.

Kuzunguka duara la rasilimali kuna maduara sita madogo yaliouganishwa na mstari mweusi. Katika duara la kwanza kuna picha ya skuli. Duara jengine dogo lina picha ya mwanamke anayeuza matunda na mboga mboga chini yake pameandikwa “Soko la Mboga mboga” na “Miche kwa ajili ya Skuli” katika mabano. Duara jengine dogo lina picha ya kanisa. Duara jengine dogo lina picha ya dereva wa bodaboda aliyepakia abiria. Chini ya picha hii pameandikwa “madereva wa bodaboda” na neno “usafiri” katika mabano. Kuna maduara mengine madogo mawili yaliounganishwa na maliasili – moja lina neno “ziwa” na jengine lina neno “ardhi”.

## Kudumisha mtandao imara wa mali za jamii

Kumbuka kuwa haitoshi tu kubaini rasilimali zilizopo katika jamii yetu. Pia hatuna budi **kujenga mtandao imara wa rasilimali** ili kuunga mkono elimu mjumisho. Tunaweza kufanya haya kwa **kuimarisha ushirikiano** baina ya Kamati za elimu mjumuisho za skuli (Kamati ya elimu mjumuisho) na rasilimali za jamii. JWU zina wajibu wa kujenga na kudumisha mitandao hii.

Kumbuka kuwa uhusiano ulio imara na shirikishi katika jamii yote ni muhimu katika kudumisha elimu mjumuisho. Kuna matendo mazuri ambayo yanaweza kusaidia kujenga ushirikiano. Pia kuna matendo mabaya ambayo yanaweza kudumaza ushirikiano huo. Ni muhimu kwetu kila siku kufikiri and kutafakari iwapo tunafanya **matendo mazuri ya kutusaidia kujenga na kudumisha ushirikiano.**




Ramani ya rasilimali iliyotengenezwa na Shirikisho la Wawezeshaji kutoka wilaya ya Sheem, Uganda.

[Ufafanuzi wa picha: Hapo juu kuna karatasi ya flipuchati iliyoandikwa Ramani ya rasilimali ya Unguja. Katikati ya karatasi hiyo kumeandikwa neno ‘rasilimali’ lililo katika duara. Kuna mistari mingi iliyoungwanishwa na visanduku vikiwa na mifano ya rasilimali, kama vile; ‘taasisi za afya’, ‘usafiri’, ‘ulinzi’ n.k.]